namna bora ya kuiomba

# SALA YA BWANA



DENIS & DEVIS

# SALA YA BWANA

**~Nuru ya upendo wa Kristo (wingulamashahidi.org)**

## Utangulizi:

Huu ni mwendelezo wa mfululizo wa miongozo maalumu ya uombaji bora, na wenye tija katika eneo la ukuaji wetu wa kiroho. Tayari tulishatoa sehemu ya kwanza hadi ya nane (1-8), ikiwa bado hujapata miongozo hiyo, basi wasiliana nasi kwa namba zetu uzionazo mwishoni kabisa mwa chapisho hili, tuweze kukusaidia.

Wapo wengi, wanatamani kweli kuomba, lakini wanapoomba hawajui waombeje, lakini pia wapo wengine ni waombaji lakini hawaombi vizuri kama vile Bwana atakavyo. Hivyo kwa miongozo hii, itakufundisha kuomba na zaidi kukuongezea vipengele muhimu vya kugusia katika uombaji wako wa sikuzote.

Leo tutapata mwongozo sahihi wa ile sala ya Bwana. Ambayo tunaisoma katika Mathayo 6:9-13. Hii ni sala iliyo ya muhimu sana, naweza kusema zaidi ya zote, kwasababu ndio tuliyofundishwa na Bwana mwenyewe na ndio aliyokuwa anaiomba yeye, na kumletea matokeo yale tunayoyaona katika huduma yake.

Lakini ijapokuwa tunaifahamu, lakini bado hatujui kuiomba ipasavyo, na hapo ndio kosa linapokuja.

Wapo watu wanaiomba kwa kurudia-rudia yale maneno, Baba yetu uliye mbingu, jina lako litukuzwe..X10, kwa siku, huku wakidhani wameshaiomba. Lakini wapo wengine wanaiomba kweli kwa kwa kunyambua –nyambua hivyo vipengele, jambo ambalo ni sahihi, lakini bado hawajui njia sahihi ya kuviomba, kiufasaha kulingana na majira yetu. Kwamfano unapoomba katika kile kipengele cha ‘ufalme wako uje’, Ukimaanisha kama ilivyoandikwa ufalme wake, uje, utakuwa upo nyuma ya wakati. kumbuka tayari ufalme wa Mungu ulishatujilia tayari (Luka 11:20). Hivyo utajikuta unaomba sala ya wakati ambao Yesu alikuwa duniani kabla ya kusulibiwa na kufufuka kwake. Ni muhimu sana kulifahamu Neno kulingana na majira.

Sasa njia sahihi ya kuiomba hii sala, kwanza ni vizuri ukafahamu yale aliyoyasema Yesu ni kama mwongozo tu, au vipengele, au ramani ya kutusaidia kuomba kiufasaha. Ili mtu akiomba asitoke nje ya maudhui ile, akaomba vitu vingine.

Ni sawa na biblia, unapoifungua tu pale mwanzoni, utaona orodha ya vitabu sitini na sita (66). Hivyo ukisema umeshaijua biblia kwa kuweza kuorodhesha kwa kuvitaja vitabu vyote, ni wazi kuwa bado hujaijua biblia. Kumbe ni lazima ujue ujumbe ulio ndani ya kila kitabu, ukishasoma na kufahamu ndio  hapo sasa utasema unaijua biblia.

Vivyo hivyo kwenye sala ile, Yesu alitoa muhtsari tu, akieleza jinsi yale maombi yake ya masafa ya  kukesha usiku kucha na yale mafupi, yote yalitembea katika mwongozo huo huo.

Na wapo wanaosema Sala hii ilikuwa ni ya kipindi kile kabla ya Yesu kufufuka, sasa hivi haina manufaa kwetu. Ukweli ni kwamba inamanufaa sana, na ni sala ya wakati wote, na vizazi vyote, isipokuwa tu wameshindwa kujua namna ya kuiomba kwa wakati wetu.

Tutaanza kunyambua kipengele kimoja baada ya kingine, na njia sahihi ya kuiomba. Katika kila kipengele tumeanisha kiwango cha dakika, ambacho ujizoeze kuomba. Kumbuka hii ni ratiba ya wiki nzima. Juma ya muda ambao utakuwa umeutumia kuomba ni SAA 7.

## SALA YA BWANA

***Mathayo 6:9 Basi ninyi salini hivi; Baba yetu uliye mbinguni,***

***Jina lako litukuzwe, Ufalme wako uje,***

***10 Mapenzi yako yatimizwe, hapa duniani kama huko mbinguni.***

***11 Utupe leo riziki yetu.***

***12 Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.***

***13 Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.***

***[Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.]***

Anaanza kusema.. tuombapo tuseme.

### 1. BABA YETU ULIYE MBINGUNI. (DK 30)

Bwana anataka tutambue kwanza maombi yetu tunayaelekeza kwa nani. Anasema Baba yetu uliye mbinguni. Kumbe ni kwa Baba na sio kwa mfalme, au Bwana, au Mola, au Yehova, au Mungu. Japokuwa vyote hivyo ni vyeo vya Mungu, lakini ametaka tulenge kwenye cheo chake cha ubaba.

Sasa katika agano jipya, Baba hakuwa tu mbinguni peke yake kama ilivyokuwa katika agano la kale. bali aliingia ndani yetu kwa Roho wake Mtakatifu, Hivyo ni sawa na kusema, “Baba yetu uliye mbinguni na uliye nasi mioyoni mwetu”...

Ukikiri hivyo, tafsiri yake ni kuwa unaeleza uwepo wa Mungu wetu kotekote, ambaye Ubaba wote wa mbingu na wa duniani unaitwa.

*Waefeso 3:14 Kwa hiyo nampigia Baba magoti,15 ambaye kwa jina lake ubaba wote wa mbinguni na wa duniani unaitwa*

Ukilijua hilo utaambatanisha na heshima yako ya kipekee, aidha kwa kupiga magoti, au kunyosha mikono yako juu, kama mwandishi alivyotenda hapo baada ya kutambua ukuu wake na uwepo wake kila mahali.

Kisha baada ya hapo fikra zako sasa zipeleke mpaka mbele ya kiti chache cha rehema. Kisha ujione kama ni mtoto kabisa kwa Baba yake, uliyestahilishwa kupokeo chochote kwake kwa neema. Anza kuuona upendo wa Mungu moyoni mwako, huruma zake, ukarimu wake, fadhili zake.

Lakini ukipoteza, imani na ujasiri uendapo kuomba katika hatua yako ya kwanza, tayari umeshaanza na mguu usio sahihi. Mungu anataka kabla ya kuomba lazima tukitambue cheo chake cha ubaba, tena sio baba tu ilimradi baba, bali Yesu alimuita “ABA” (Marko 14:36)

Aba ni Yule baba mwenye mahusiano na mwanawe ya karibu sana kana kwamba ni mtu na rafiki yake, vilevile Yule baba mwenye huruma sana iliyopitiliza kwa mtoto wake,asiyependa kumwona yupo katika hali ya dhiki.

*Zaburi 103:3 Kama vile baba awahurumiavyo watoto wake, Ndivyo Bwana anavyowahurumia wamchao. 14 Kwa maana Yeye anatujua umbo letu, Na kukumbuka ya kuwa sisi tu mavumbi. 15 Mwanadamu siku zake zi kama majani; Kama ua la kondeni ndivyo asitawivyo.*

- ✓ Mungu hataki tuendapo kuomba tuwe wanyonge kama mayatima, tusiosikilizwa na mtu. Hataki hilo, hivyo usiruhusu kuomba kihofu –hofu tu, yaani kuomba kama vile wewe ni mgeni mbele zake, unapaswa upokee ujasiri wake, kama vile wewe umerudi nyumbani kwenu, kwa baba yako akupendaye sana.

Ni kawaida kujiona mkosaji, mbele zake, ndivyo ilivyokuwa kwa Yule mwana –mpotevu, lakini hakuwaza vyema kwa baba yake. Kinyume chake, aliona mwitikio wa ajabu badala ya kugombezwa, alihurumiwa sana, na kufanyiwa karamu. Vivyo hivyo na sisi, tunafanyiwa karamu karamu kubwa na Baba yetu pale tunapomwendea kwa moyo wa dhati kabisa kumwomba lolote.

***Hii ni hatua ya kwanza, jihudhurishe kama mtoto apendwaye kabisa.***

Baada ya hapo anasema tuombe.

## 2. <u>JINA LAKO LITUKUZWE. (Dk 60)</u>

Hicho ndio kipengele cha kwanza unachopaswa kuomba. Sasa ni kwanini Bwana Yesu alitaka tuombe jina la Mungu litukuzwe, kwani lisingeweza kutukuzwa tu lenyewe ndani yetu bila kuomba?

Ni kutuonyesha kuwa uwezekano wa kutotukuzwa jina lake upo tukajitukuzwa sisi, au vitu vingine, Na hilo sio kusudi la Mungu kutuumba . Alituumba kwa ajili yake, ili kila kitu duniani au tukifanyacho kilitukuze jina lake.

Sababu mojawapo ya watu wa Babeli kuangushwa ilikuwa ni kujiundia wao jina lao, ili watukuzwe na sio Mungu. Yaani wawe na jina duniani, lakini sio Mungu, ndio sababu wakasambaratishwa.

*Mwanzo 10:1 Nchi yote ilikuwa na lugha moja na usemi mmoja.  2 Ikawa watu waliposafiri pande za mashariki waliona nchi tambarare katika nchi ya Shinari; wakakaa huko.  3 Wakaambiana, Haya, na tufanye matofali tukayachome moto. Walikuwa na matofali badala ya mawe, na lami badala ya chokaa.  4 Wakasema, Haya, na tujijengee mji, na mnara, na kilele chake kifike mbinguni, TUJIFANYIE JINA; ili tusipate kutawanyika usoni pa nchi yote.  5 Bwana akashuka ili auone mji na mnara waliokuwa wakiujenga wanadamu.  6 Bwana akasema, Tazama, watu hawa ni taifa moja, na lugha yao ni moja; na haya ndiyo wanayoanza kuyafanya, wala sasa hawatazuiliwa neno wanalokusudia kulifanya.  7 Haya, na tushuke huko, tuwachafulie usemi wao ili wasisikilizane maneno wao kwa wao*

<u>Je! Jina la Mungu linatukuzwa wapi?</u>

I. ***<u>Kupitia vivywa vyetu:</u>***

- ✓ Hivyo omba Mungu akupe ujasiri wa kumkiri yeye, popote uwapo, bila kumwonea aibu. Mfano wa Daudi alivyosema;

Zaburi 119:46 Nitazinena shuhuda zako mbele ya wafalme, Wala sitaona aibu

- ✓ Mwombe Bwana akupe kinywa cha sifa, wakati wote uwe na bubujiko la kumsifu Mungu kwa ukuu wake, na wema wake, na uweza wake.

Zaburi 150: 6 Kila mwenye pumzi na amsifu Bwana. Haleluya.

II. ***<u>Karama zetu:</u>***

Kwa mfano umepewa karama Fulani labda ya uponyaji, Pale unapomponya mtu ni rahisi sana kuchukua utukufu wa Mungu. Hapo ni kuwa makini na kumwomba Mungu katika karama au neema yoyote aliyokupa basi utukufu wote, ujapo umrudie yeye. Wengi wamechukua utukufu wa Mungu kwa namna hii, na hivyo ikawapelekea Mungu kuwashusha chini, au utukufu wa Mungu kufichwa., haijalishi wewe ni mchungaji, mwinjilisti, nabii, una karama ya maarifa, masaidiano. N.k. Ni kuomba Bwana akupe macho ya kumrejeshea utukufu kwa kipawa ulichopewa.

Tusiwe kama Musa na Haruni walivyofanya kwa wana wa Israeli, mpaka ikawapelekea nao wao pia kutoiona nchi ya ahadi, kwa kosa tu la kuchukua utukufu wa Mungu.

### ***III. Matendo yetu:***

Omba Bwana akupe kiu ya kutembea katika mwenendo mzuri

Maandiko yanasema..

1Petro 2:12 Mwe na mwenendo mzuri kati ya Mataifa, ili, iwapo huwasingizia kuwa watenda mabaya, wayatazamapo matendo yenu mazuri, wamtukuze Mungu siku ya kujiliwa.

### ***IV. Nguvu zetu na Akili zetu.***

Ni lazima tuombe, fedha zetu, mali zetu, kazi zetu zitumike kuifanya kazi ya Mungu, vilevile zilete sifa njema kwa Mungu. Hivyo tuombe utambuzi wa jambo hili kila wakati ili zitende kazi ya Mungu sio yetu.

Vilevile sisi kama wanadamu tumepewa akili za kubuni, kuvumbua, na kuunda, sasa ni rahisi tukatukuzwa sisi kwa mambo yetu maridadi tuliyopewa. Utaona wengine wanajisifia teknolojia zao, majengo yao n.k.badala ya kumtukuza Mungu aliyewapa akili hizo.

### ***V. Maumbile yetu:***

Wakati mwingine Mungu anaweza kuweka kitu cha kitofauti, kimwonekano, mwilini mwako ambacho kikakupelekea iwe rahisi watu kukusifia wewe badala ya Mungu, labda utakuta ni nywele nzuri, au macho mazuri, au sauti nzuri n.k. Vitu kama hivi katika maumbile yetu, Mungu ameviweka kwa utukufu wake sio sisi. Hivyo mwombe Mungu akupe wepesi wa kuelekeza utukufu wote kwake, kwa kila kitu cha kipekee ulichonacho, pindi watu wanapokusifia

### ***VI. Imani zetu:***

Hapa ni kuomba Mungu akuongezee imani, kwasababu imani yako iwapo kubwa kwake, utatenda mambo makuu kwa jina lake, na hivyo atatukuzwa Mungu. Eliya alisababisha jina la Mungu kutukuzwa pindi aliposhusha moto mbele ya miungu baali, Daudi alilisababishia jina la Mungu kutukuzwa, pindi alipomwangusha Goliati, Vivyo hivyo na wewe utafanya jina la Mungu litukuzwe imani yako inapotenda kazi.

### ***VII. Jamii yetu:***

Hapa ni kuombea mazingira yatuzungukayo, hususani katika nyakati hizi za mwisho za hatari, watu wamemkinai Mungu, kila jambo ambalo linaonekana wazi kabisa kwamba ni kazi ya Mungu, watu husema hakuna Mungu bali ni vitu tu vya asili vimejizukia, vimetokea kwa asili. Hivyo ni kuombea sana, jamii yako, familia yako, nchi yako

visijikuze kwa chochote bali wamtukuze Mungu katika yote. Mungu aliliangamiza taifa la Tiro na mkuu wao kwasababu lilijitukuza lenyewe, juu ya Mungu. (Ezekieli 28)

## 3. UFALME WAKO UJE. (dk 60)

Tunapoomba maombi haya, hatuombi. Kwamba ufalme wa Mungu, uje duniani, kwasababu kwa sisi wa Agano jipya tayari tumeshajiliwa na Ufalme wa Mungu (Luka 11:20). Kupitia Roho Mtakatifu siku ile ya Pentekoste. Hivyo lazima tufahamu tunapaswaje kuomba ombi la namna hii.

Jinsi ya kuomba:

- ✓ ***Ufalme wake uje maana yake, Ufalme wake uenee.***Watu wakasikie habari za injili, kotekote, hivyo Bwana akanyanyue zana za kazi, ikiwemo,
- ✓ ***Watenda kazi:*** (Mathayo 9:38)
- ✓ ***Fedha kwa wapeleka injili:*** (Warumi 10:15)
- ✓ ***Watu wa amani:*** Hawa ni wakaribishaji wa wapeleka injili. Ndio wale Yesu aliosema katika;

*Mathayo 10:12 Nanyi mkiingia katika nyumba isalimuni. 13 Na nyumba ile ikistahili, amani yenu na iifikilie; la, kwamba haistahili, amani yenu na iwarudie ninyi.*

Mfano wa Hawa ndio wale wakina Lidia, Prisila na Akila, Onesmo, Gayo n.k. Ni muhimu sana kuomba Mungu awanyanyue watu wengi kama hawa katika kupeleka kwetu injili kwasababu ndio wanakuwa malimbuko hasaa ya makanisa mahali mahali, wakikosekana injili huwa inatumia nguvu kubwa zaidi kupenya maeneo hayo.

- ✓ ***Tunaomba pia kuulewa ufalme wa Mungu zaidi na zaidi***. Kwa kujua namna ya kuzitumia funguo zake vizuri. Tunaweza kweli tukawa na ufalme wa Mungu moyoni mwetu, lakini tusijue namna ya kuuachilia njia. Hivyo ni kuomba Bwana atupe hekima, busara na maarifa katika kuhubiri wetu na kuipeleka mbali.
- ✓ ***Vilevile tunaomba vizuia injili vidhibitiwe.***

1Wakorintho 16:9 kwa maana nimefunguliwa mlango mkubwa wa kufaa sana, na wako wengi wanipingao.

Wakati mwingine Paulo alitamani kuwarejea tena watu wa Rumi, kwa mara mbili lakini shetani akamzuia(1Wathesalonike 2:18). Hivyo ni kuomba utisho wa Bwana, na nguvu za Mungu ziwepo kukinzana na wapingamizi wa injili.

- ✓ ***Matendo ya ufalme kama vile Ishara na miujiza yakatendeke.***

Miujiza ishara na maajabu, ni chambo kubwa sana ya injili kuenea kwa kasi, Pale watu wanapoona ishara nyingi zinatendeka, hugeuka kiwepesi. Kanisa la kwanza lilitumia wakati mwingi kuomba jambo hili, na hivyo Mungu akawajalia mambo hayo.

Matendo 4:30  ukinyosha mkono wako kuponya; ishara na maajabu vifanyike kwa jina la Mtumishi wako mtakatifu Yesu. 31  Hata walipokwisha kumwomba Mungu, mahali pale walipokusanyika pakatikiswa, wote wakajaa Roho Mtakatifu, wakanena neno la Mungu kwa ujasiri.

Ukigusia vipengele hivyo vyote, utakuwa umeomba vizuri, kwenye maeneo muhimu ya ufalme wa Mungu.

## 4. MAPENZI YAKO YATIMIZWE. (dk 60)

Kwanini Bwana atuagize kuomba mapenzi yake yatimizwe?. Ni kwasababu alijua pia upo uwezekano wa sisi kutembea nje ya mapenzi yake. Na hivyo alitaka  tufanye bidii sana kuomba ili tuweze kutembea katika hayo mapenzi yake, vinginevyo hatutaweza.

Kwa kawaida mwanadamu yoyote, si mwepesi kuitikia mapenzi ya Mungu, kwasababu vinakinzana sana na matamanio yetu, Kwamfano Mungu anakuambia uombe, lakini nafsi yako inakuambia umechoka. Hivyo ni vita vikubwa.

Mfano halisi ni Bwana wetu Yesu Kristo, yeye mwenyewe alijaribu kushindana na kusudi la Baba yake, pale alipotaka kikombe cha mateso kimwepuke, lakini tuona jinsi gani alivyokuwa mnyenyekevu akamalizia kusema “si kama mimi nitakavyo lakini mapenzi yako yatimizwe”.(Mathayo 26:42)

Yeye alitaka astarehe, asipigwe, lakini Mungu alikusudia apigwe kwa ajili yetu.

Vipi ikiwa hali unayopitia isiyokupendeza ni mapenzi ya Mungu, halafu wewe unashindana nayo, Unahitaji kuomba sana, ili uwe na amani anapokupitisha katika mapito yake usiyoyaelewa wewe kwa ufahamu wako.

- ✓ ***Hivyo omba Mungu akupe kuyaona, kuyatambua na kuyakubali mapenzi yake yote aliyokuagiza.***

Lakini mapenzi ya Mungu pia ni wewe,<u>*Uuweze mwili wako, katika utakatifu.*</u>

1Wathesalonike 4:3  Maana haya ndiyo mapenzi ya Mungu, kutakaswa kwenu, mwepukane na uasherati; 4  kila mmoja wenu ajue kuuweza mwili wake katika utakatifu na heshima; 5  si katika hali ya tamaa mbaya, kama Mataifa wasiomjua Mungu.

Si kawaida ya binadamu kujidhibiti mwenyewe, apende utakatifu. Atapenda aupe mwili wake chochote apendacho yeye. Lakini mapenzi ya Mungu sio kuupa mwili chochote utakacho bali kile Mungu atakacho. Mungu anapenda uvae mavazi ya kujisitiri, Mungu hapendi uzinzi, Mungu hapendi uubadili mwili wako, kwa mapambo ya ulimwengu huu.

- ✓ ***Hivyo omba akupe moyo, wa kupenda utakatifu ili uyatimize mapenzi yote ya Mungu .***

Mpenzi ya Mungu pia ni Yesu ajulikane ulimwenguni. Hivyo omba neema ya kumwelewa na kumhubiri vema Yesu katikati ya watu wasioamini, waokoke. Usihubiri injili ya akili yako mwenyewe.

Yohana 6:40  Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila amtazamaye Mwana na kumwamini yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho.

## 5. UTUPE LEO RIZIKI YETU. (dk 60)

Hili ndio eneo la mahitaji yetu,

Hapa tunampelekea Mungu, haja zetu zote, siku kwa siku. Ni mapenzi ya Mungu kuwa tuombe. Tusipuuzie tukasema Mungu anajua haja zetu atatupa tu, ni kweli anajua haja zetu, lakini hilo halimaanishi tusiombe. Alisema hivyo kutuambia kuwa tusivisumbukie hivyo, yaani tusipoteze nguvu zetu kuviwaza, lakini sio kwamba tusimweleze kabisa haja zetu hapana, Peleka mahitaji yako kwa Bwana katika maeneo yafuatayo;

- ✓ ***Chakula bora:*** Omba akupe, na pia usipungukiwe chakula wewe na nyumba yako.
- ✓ ***Malazi mazuri:*** Nyumba, nzuri, mahali pa utulivu utapaomwambudia Mungu wako.
- ✓ ***Afya:*** Wewe na familia yako
- ✓ ***Kazi:*** Halali na Itakayokupa kipato kizuri cha kuendelea vema maisha yako
- ✓ ***Fedha:*** Ya kumudu mahitaji mengine mbalimbali yaliyo moyoni mwako

Utagusia na maeneo mengine yote ya mahitaji yako.

## 6. UTUSAMEHE MAKOSA YETU (dk 60).

*Mathayo 6:12  Utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu.*

Sisi kama watoto wa Mungu tunamkosea sana Mungu kwa namna nyingi. Na hivyo kila wakati hatuna budi kumwomba Mungu atusamehe. Lakini angalia anavyosema hapo  , “kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu”.

Kwa lugha rahisi, sentensi hiyo tunaweza sema, “Mungu hutusamehe makosa yetu, pale tunapowasamehe wengine.”

Hivyo anachotaka hasaa kwetu hapo sio tumtazame yeye kutusamehe, bali tutazame wengine kuwasamehe na yeye mwenyewe tu atatusamehe sisi.

Kwa ombi la hapa. Ni kujiombea hasa wewe.

Je tunaombaje?

- ✓ ***Bwana atupe moyo wa kuachilia na*** kusamehe kama alivyosema hata mara saba sabini: Uchungu wote kinyume na wale waliokukosea, uondoke ndani yako. Vilevile uwe mwepesi wa kutoshikilia mambo moyoni mwako.
- ✓ ***Akuondolee moyo wa kuhesabu mabaya.***
- ✓ ***Akupe upendo wa kuwaambea wale wanaokuudhi na hata maadui zako.***
- ✓ ***Uwe si mwepesi wa hasira.***
- ✓ ***Akupe moyo wa uvumilivu.***

Ukizingatia hayo, basi Mungu naye atakusamehe dhambi zako. Usitumie muda mwingi hapo kutubu, la kuomboleza, tumia muda mwingi, kuomba juu ya nafsi yako iwe na moyo wa kusamehe. Hiyo ndio namna bora ya kuomba Mungu akusamehe wewe.

## 7. <u>USITUTIE MAJARIBUNI. (dk 60)</u>

*Mathayo 6:13 Na usitutie majaribuni, lakini utuokoe na yule mwovu.*

Yesu aliona pia umuhimu wa kuomba ulinzi,

Maandiko yanasema shetani ni kama simba angurumaye atafutaye mtu wa kummeza. Ijapokuwa tumemshinda kwa kifo cha Kristo pale msalabani, hatupaswi kudhani kuwa haangahiki tena kutusumbua, endapo tutalegea.

Hivyo kuomba kwetu dhidi ya shetani baada ya Yesu kufufuka, hakuwi tena kumwachia Mungu amfukuze, bali ni kushughulika naye sisi wenyewe, kwa mamlaka tuliyopewa katika jina la YESU KRISTO, kuangusha na kuharibu kazi zake zote.

Mathayo 10:19 Tazama, nimewapa amri ya kukanyaga nyoka na nge, na nguvu zote za yule adui, wala hakuna kitu kitakachowadhuru.

- ✓ ***Tumia mamlaka uliyonayo kuangusha kuta, ngome na kufukuza kila pepo, kwa jina la Yesu linalosogelea eneo lako lolote lile, iwe ni katika***

Wokovu wako na huduma yako au Afya yako, Au Familia yako, Au Uchumi wako.

Usipokuwa mwombaji, na kuvunja na kung'oa mapando ya mwovu maishani mwako, shetani atakusaidia kupanda na kupalilia yeye mwenywe shamba lako. Kwahiyo kemea, tumia kinywa chako, kunena maneno yenye mamlaka dhidi ya hila zote za mwovu.

Na mwisho Bwana anasema..

## 8. KWA KUWA UFALME NI WAKO NA NGUVU. (dk 30)

Mathayo 6:13:...[Kwa kuwa ufalme ni wako, na nguvu, na utukufu, hata milele. Amina.]

Hii ni sala ya kumwadhimisha Bwana ajibuye maombi, sio saa ya kupeleka mahitaji, hapana , ni sala ya kuutangaza ukuu wake wote, unamwambia Bwana wewe ni mkuu, Wewe ni mwema, , duniani hayupo Mungu kama wewe, mbinguni hajawahi kuwepo, unamiliki vyote, vimetoka kwako na vitarudi kwako, Wewe ni Mungu mwenye kutisha, dunia nzima inatetemeka mbele zako, viumbe vyote vinakushukuru. Kwani utukufu wote ni wako, ufalme wote si wetu ni wako,.

Na maneno mengine kama hayo, kwa jinsi Roho atakavyokuongoza..

- ✓ Na jambo la muhimu sana ,kumwinua Mungu wako, Eleza wema wake, uweza wake kwa jinsi uwezavyo, Kwa jinsi Bwana anavyokujalia, Tumia muda mwingi kufanya hivyo.

**Zingatia:** Kuomba kwa Roho Mtakatifu (kunena kwa lugha), pia kwafaa sana kwa maombi yote. Mpe nafasi Roho kukuombea vizuri, kwasababu yeye ndiye ayakamilishaye maombi yetu.

Na kwa kufanya hivyo utakuwa umeomba sawasawa na Bwana aombavyo.

Bwana akubariki.

Mwendelezo unakuja...

**Kwa Mawasiliano:**

~Mwl Denis & Devis Julius
Nuru ya Upendo wa Kristo
Piga/Whatsapp:+255 693036618 / +255 789001312
www.wingulamashahidi.org